



# Maua kwa ajili ya Jirani Yangu



**Na Petro E., umri miaka 10, Utah, Marekani**

Miaka michache iliyopita, mume wa jirani yangu alifariki. Mke alikuwa na huzuni sana.

Nilijua vile inavyokuwa kwa kumpoteza mtu unayempenda. Nilipokuwa na umri wa miaka mitatu, mama yangu alifariki. Baada ya kufariki, watoto katika ujirani wangu walimwandikia kaka yangu pamoja na mimi barua na wakapamba baraza yetu na wanasesere. Nilitaka kufanyia jambo fulani zuri tu kwa ajili ya jirani yangu.

Nilisali ili kujua ninapaswa kufanye nini ili kusaidia. Wazo lilinijia kichwani la kumpa maua siku ya Wapendanao. Hata hivyo, nilihitaji kupata pesa kununua maua. Nilifanya iwe lengo katika *Kitabu cha Mwongozo cha Watoto* cha kwangu ili kupata pesa.

Nilipata pesa kwa kufanya kazi tofauti kwa wengine. Bibi yangu alinilipa kusafisha bustani yake na majani katika baraza yake. Nyumbani, nilipata pesa kwa kusafisha vichaka nyuma ya banda letu. Ilichukuwa miezi ya kazi ngumu kupata pesa ya kutosha.

Hatimaye nilikuwa na pesa za kutosha kwenda kwenye duka na kununua maua. Ikaja Siku ya Wapendanao, na nilimpa jirani yangu yale maua na barua. Alifurahi sana. Nilijihisi ukunjufu na furaha pia. Nilimshukuru Baba wa Mbinguni kwa kunisaidia kufanya kile Yeye alichotaka mimi nifanye. ●